**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

2024-03

# Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha Akiwasilisha Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti Ya Serikali Kwa Mwaka 2024/2025

Jamhuri ya Muungano, Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/835

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25**

**11 MACHI 2024**

## MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (Mb), WAZIRI WA FEDHA AKIWASILISHA KATIKA KAMATI YA BUNGE ZIMA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

### UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*,** napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad H. Chande (Mb), Katibu Mkuu Dr. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Wakuu, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya usimamizi wa masuala ya uchumi na fedha pamoja na ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya shughuli za Serikali. Vilevile, nitumie fursa hii kutoa salamu zangu za pole kwa Mhe. Rais na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi pamoja na Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa. Kadhalika, natoa pole kwa watanzania wote walioathirika na mvua za Elnino zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Sambamba na hilo, Serikali inaendelea kurejesha miundombinu iliyoharibiwa ili kuhakikisha huduma za jamii na kiuchumi zinarejea katika hali ya kawaida.

3. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*,** ninawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la Februari, 2023. Aidha, taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/24; Sehemu ya Tatu ni Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/25; na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

### MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2023/24

4. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*,** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha bajeti ya Serikali ya shilingi bilioni 44,388.1 kwa mwaka 2023/24 kutekeleza dhima ya Taifa ya "Kuchochea Kasi ya Ukuaji wa Uchumi, Kuhimili na Kukabili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji ili Kuboresha Hali ya Maisha ya Wananchi". Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 29,172.5 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,215.6 ni matumizi ya maendeleo. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza dhima ya Taifa kwa: kuongezea ushiriki wa sekta binafsi nchini; kuendelea kuimarisha sekta za uzalishaji zinazoajiri

wananchi wengi nchini; na kugharamia athari za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza.

5. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika licha ya kukumbwa na changamoto kadhaa ambazo baadhi zinatokana na sababu ambazo ziko nje ya uwezo wa Serikali kama vile mabadiliko ya tabianchi, athari za vita na mabadiliko ya kisera za nchi zilizoendelea ikiwemo sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika uchumi (Tightening Monetary Policy). Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2023, ukuaji wa uchumi wa Taifa ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Katika mwaka mzima wa 2023 (Januari – Desemba), uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 4.9 mwaka 2022.

6. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi ni matokeo ya uongozi thabiti wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchukua jitihada mbalimbali za kukuza uchumi ikiwemo: Kuimarisha mazingira ya utawala bora na utawala wa sheria; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, hususan utashi wa kisiasa wa kuruhusu mijadala na mashauriano ya masuala ya uwekezaji kwa wadau wa ndani na nje; kuongeza rasilimali fedha katika sekta za uzalishaji na huduma za jamii, na utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye matokeo ya haraka katika ukuaji wa uchumi; na kuendelea kutoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoibuliwa na Serikali.

7. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ambao ni ndani ya lengo la nchi la wastani wa kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0. Kudhibitiwa kwa mfumuko wa bei kumetokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania katika kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuhakikisha nchi inakuwa na utoshelevu wa chakula wenye kumudu mahitaji ya soko la ndani na la nchi jirani. Kiwango cha utoshelevu wa chakula kimeongezeka kufikia asilimia 124 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 114 mwaka 2022/23;
(ii) Kuhakikisha upatikanaji wa mbolea ambapo tani 418,942 ziliuzwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku katika mikoa 26 ili kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima (imported inflation) na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora na mazao;
(iii) Kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ili kuhakikisha mazao yanasafirishwa kwa gharama nafuu kutoka maeneo ya uzalishaji vijijini hadi maeneo ya walaji, hususan masoko ya mijini; na
(iv) Utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

## Mwenendo wa Mapato

### Mapato ya Ndani

8. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Januari 2024, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 17,188.4, sawa na asilimia 95.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 17,929.8 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23, sawa na ukuaji wa asilimia 10.0. Kati ya mapato hayo: mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi bilioni 15,159.8, sawa na asilimia 97.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 15,492.7; mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,374.5; na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 654.1.

9. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika kipindi kilichobaki hadi Juni 2024, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo:

(i) Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka nchini kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo;
(ii) Kuendelea kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kufuatilia kiasi halisi cha kodi kinachopaswa kulipwa na walipakodi;
(iii) Kuongeza usajili wa walipakodi na usajili wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kupitia usimamizi bora wa vitalu na kampeni za mlango kwa mlango;
(iv) Kuendelea kufanya maboresho ya mifumo ya ukusanyaji wa kodi ili kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika matumizi ya mifumo na kuifanya kuwa rafiki kwa walipakodi; na
(v) Kuimarisha usimamizi wa kodi ya zuio kwa taasisi za Serikali kupitia mpango jumuishi na endelevu wa ushirikishaji.

### Misaada na mikopo

10. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika mwaka 2023/24, Serikali ilipanga kukopa katika soko la ndani shilingi bilioni 5,440.4. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,898.3 ni kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti na shilingi bilioni 3,542.1 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani zilizoiva. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Januari 2024, Serikali imekopa shilingi bilioni 2,757.5, sawa na asilimia 84.7 ya makadirio ya kukopa shilingi bilioni 3,254.9. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,716.27 zimetumika kulipa hatifungani zilizoiva na shilingi bilioni 1,041.23 zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo.

### Mwendendo wa Matumizi

11. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Januari 2024, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 27,286.0. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,771.4 ni mishahara, shilingi bilioni 5,815.2 ni ugharamiaji wa deni la Serikali, shilingi bilioni 4,253.6 ni uendeshaji wa shughuli za Serikali na shilingi bilioni 11,445.8 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

12. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha Julai 2023 hadi Januari 2024 chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na:

(i) Kuchachua uchumi kwa kuwezesha malipo ya mishahara ya watumishi wa umma kwa wakati;

(ii) Kugharamia deni la Serikali kadiri linavyoiva ambapo imewezesha Serikali kuendelea kuimarisha nidhamu ya usimamizi wa deni;

(iii) Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi ambapo jumla ya shilingi bilioni 430.6 zimetolewa na kunufaisha wanafunzi 222,131 wa elimu ya juu na wanafunzi 1,429 wa ngazi ya stashahada;

(iv) Utolewaji wa elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari ambapo jumla ya shilingi bilioni 233.1 zimetolewa na kunufaisha wanafunzi 2,815,087 wa sekondari na wanafunzi 12,388,118 wa shule za msingi;

(v) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za kijamii, hususan maji, afya na elimu;

(vi) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa asilimia 10.0; na

(vii) Kuendelea kugharamia miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa Reli ya kisasa (SGR) pamoja na utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme ambapo tayari vichwa vya treni vya umeme vinne (4) vimepokelewa na kuanza majaribio; pamoja na bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere ambapo hatua iliyofikiwa ni kuanza majaribio na kuunganishwa kwa mtambo mmoja (1) wenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kwenye gridi ya Taifa mwezi Februari 2024.

## MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

### Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

13. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2024/25 ni:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.7 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.5 mwaka 2023/24;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 2.8 ya mwaka 2023/24; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

14. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 yameandaliwa kwa kuzingatia misingi ya uchumi jumla ambayo ni:

(i) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara kwa kuboresha miundombinu wezeshi (barabara, reli, nishati, maji) na kuimarisha misingi ya usimamizi wa Sera ya Ushirikishaji wa Wazawa (Local Content Policy) kwenye miradi inayogharamiwa na Serikali);

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko n.k;

(iii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

**Sera za Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2024/25**

15. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** sera za mapato na hatua za kiutawala kwa mwaka 2024/25 zitalenga kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuendelea kutekeleza yafuatayo: Kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari; kuongeza wigo wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato, hususan kodi ya ardhi na pango.

16. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Lengo ni kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikijumuisha mishahara na deni la Serikali. Aidha, Serikali itaendelea kugharamia matumizi ya maendeleo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa Taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji na Wakala wa Maji Vijijini. Vilevile, Serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai pamoja na kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na kuendana na thamani ya fedha.

**Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2024/25**

17. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali itatoa kipaumbele katika kugharamia miradi na programu za maendeleo zinazoendelea kabla ya kuruhusu usajili wa miradi mipya. Aidha, ukomo wa bajeti kwa mafungu umezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25. Maeneo mengine ya kipaumbele yatajumuisha ugharamiaji wa: maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; deni la Serikali; mishahara; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025; ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya Michuano ya Mpira wa Miguu ya Mataifa ya Afrika (AfCON) ya mwaka 2027; huduma za jamii; na sekta za uzalishaji.

## Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/25

**Mapato**

18. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali inapendekeza bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 49,345.7 kwa mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 11.2 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24 ya shilingi bilioni 44,388.1. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 29,858.4, mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Taasisi na Idara zinazojitegemea shilingi bilioni 3,408.1; na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 1,344.1.

19. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** makadirio ya mapato kwa mwaka 2024/25 yamezingatia vigezo mbalimbali ikiwemo mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato; mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla; na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Aidha, sehemu kubwa ya bajeti (asilimia 70.1) itagharamiwa na mapato ya ndani ambayo yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 10.0 mwaka 2024/25. Hivyo, Serikali itaendelea kuweka msukumo na jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuwa ndicho chanzo chenye uhakika na kisicho na masharti hasi katika kugharamia bajeti ya Serikali.

20. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ongezeko la mapato ya ndani limetokana na hatua mbalimbali za kiutawala na kisera zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti ya Chama cha Mapinduzi katika kusimamia ukusanyaji wa mapato. Hatua hizo zinajumuisha: uanzishaji wa Tuzo ya Uzalendo ambayo maandalizi yake yapo katika hatua za mwisho; uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, ikiwemo mfumo wa uthaminishaji wa mizigo wa forodha (TANCIS) ambao utafungamanishwa na mfumo wa kodi za ndani (IDRAS); kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi (less cash) ikiwemo matumizi ya mfumo wa malipo ya kielektroniki (Tanzania Instant Payment System) utakaopunguza gharama za miamala; kuendelea kuwekeza katika sekta za

uzalishaji na maeneo yenye matokeo ya haraka (quick wins) ili kuongeza wigo wa kodi; kuendelea na hatua za urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; kutoa elimu ya mlipakodi kwa umma ili kuongeza uhiari wa kulipa kodi; na kuendelea kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi ikijumuisha uboreshaji wa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mipakani (OSBP). Aidha, Serikali inakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Muda wa Kati wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani utakaoainisha hatua mbalimbali za kuongeza mapato ya ndani.

21. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 5,130.6. Aidha, Serikali inakadiria kukopa shilingi bilioni 6,617.8 kutoka soko la ndani ambapo shilingi bilioni 4,022.4 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi bilioni 2,595.4 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inakadiria kukopa shilingi bilioni 2,986.6 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) itaendelea kuhakikisha kuwa fedha za mikopo zinaelekezwa kwenye miradi ya kimkakati yenye matokeo ya haraka (quick wins) na manufaa mapana kwa Taifa (multiplier effect) ikiwemo kuongeza fursa za ajira na wigo wa mapato ya Serikali na kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati.

**Matumizi**

22. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kuhakikisha kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inafikiwa, Serikali kwa mwaka 2024/25 inapanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 49,345.7 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na ongezeko la asilimia 11.2 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 33,556.6 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,789.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Fedha za maendeleo zinajumuisha ruzuku ya maendeleo ya shilingi bilioni 1,234.1 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya kati na ya juu pamoja na programu ya elimumsingi na sekondari bila ada.

23. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** sehemu kubwa ya matumizi itaelekezwa katika kugharamia deni la Serikali, mishahara ya watumishi wa umma, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, ulipaji wa hati za madai pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya Michuano ya Mpira wa Miguu ya Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027. Aidha, utengaji wa fedha za maendeleo umezingatia miradi inayoendelea ikiwemo miradi ya kimkakati na ya kielelezo pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa PPP ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka.

24. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa mwaka 2024/25 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**:

**Jedwali Na.1: Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25**

| | | | Shilingi Milioni | % |
|---|---|---|---|---|
| | Mapato | BAJETI ILIYOPITISHWA 2023/24 | BAJETI INAYOPENDEKEZWA 2024/25 | BADILIKO |
| A. | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | **30,237,128** | **33,266,523** | 10.0% |
| | (i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi (TRA) | *26,725,409* | *29,858,410* | 11.7% |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | *3,511,719* | *3,408,114* | -3.0% |
| B. | **Mapato ya Halmashauri** | **1,143,883** | **1,344,123** | 17.5% |
| C. | **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | **5,466,215** | **5,130,613** | -6.1% |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | *2,184,134* | *1,489,775* | -31.8% |
| | (ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | *3,151,958* | *3,513,958* | 11.5% |
| | (iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | *130,123* | *126,881* | -2.5% |
| D. | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **7,540,840** | **9,604,428** | 27.4% |
| | (i) Mikopo ya Nje | *2,100,464* | *2,986,638* | 42.2% |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | *1,898,316* | *2,595,417* | 36.7% |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | *3,542,061* | *4,022,373* | 13.6% |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | **44,388,067** | **49,345,688** | 11.2% |
| | | | | |
| | Matumizi | | | |
| E. | **Matumizi ya Kawaida** | **29,172,478** | **33,556,566** | 15.0% |
| | | | | |
| | o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | 13,084,572 | 15,736,279 | 20.3% |
| | o/w Malipo ya Riba Ndani | *2,799,374* | *3,146,668* | 12.4% |
| | o/w Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | *3,542,061* | *4,022,373* | 13.6% |
| | o/w Malipo ya Mtaji Nje | *2,763,947* | *3,517,120* | 27.2% |
| | o/w Malipo ya Riba Nje | *1,364,377* | *2,435,305* | 78.5% |
| | (ii) Mishahara | *10,882,126* | *11,997,752* | 10.3% |
| | (iv)Matumizi Mengineyo (OC) | *5,205,780* | *5,822,535* | 11.8% |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri (own source) | *689,468* | *801,563* | 16.3% |
| | | | | |
| F. | **Matumizi ya Maendeleo** | **15,215,589** | **15,789,122** | 3.8% |
| | (i) Fedha za Ndani | *11,933,508* | *12,148,283* | 1.8% |
| | o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *528,000* | *400,000* | -24.2% |
| | o/w Mfuko wa Reli na Maji na REA | *1,058,280* | *1,274,613* | 20.4% |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri (own Source) | *454,415* | *542,560* | 19.4% |
| | o/w Ruzuku ya Maendeleo | *1,138,369* | *1,234,061* | 8.4% |
| | - HESLB | *738,727* | *832,420* | 12.7% |
| | - Elimu Msingi na Sekondari bila ada | *399,642* | *401,640* | 0.5% |
| | o/w Miradi mingine | *8,754,444* | *8,697,050* | -0.7% |
| | (ii) Fedha za Nje | *3,282,081* | *3,640,838* | 10.9% |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | **44,388,067** | **49,345,688** | 11.2% |
| | **NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)** | **-2.8%** | **-2.9%** | |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**HITIMISHO**

25. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2024/25 yatakuwa ni ya nne katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Maeneo ya vipaumbele yatakayozingatiwa ni kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25, hususan ukamilishaji wa miradi inayoendelea ili kukamilika kwa wakati. Aidha, kipaumbele ni kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikiwemo malipo ya deni la Serikali, mishahara, hati za madai na ugharamiaji wa huduma za kijamii.

26. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kuimarisha mifumo na mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kugharamia sehemu kubwa ya matumizi yake kwa kutumia mapato ya ndani. Nitoe rai kwa watanzania wote kuona umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari kwani mapato hayo ndiyo yanayoiwezesha Serikali kusogeza karibu huduma muhimu kwa wananchi ikiwemo barabara, shule, vituo vya afya, maji na huduma za ugani. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na sheria nyingine kwa lengo la kuelekeza fedha kwenye utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa. Vilevile, natoa rai kwa mafungu kuzingatia katika bajeti ya 2024/25 mahitaji ya ukamilishaji wa miradi inayoendelea na yenye matokeo ya moja kwa moja kwenye uchumi na ustawi wa wananchi walio wengi. Kadhalika, mafungu yazingatie sera ya uzawa katika ushirikishaji wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji, biashara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kibiashara kwa utaratibu wa PPP ili kupunguza gharama zinazoweza kuepuka katika bajeti ya Serikali.

27. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** naomba kuwasilisha.